TANGAZO LA SERIKALI Na. 79 la tarehe

SHERIA YA MIPANGO MIJI,
(SURA YA 355)

---

**AMRI**

---

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

---

AMRI YA MIPANGO MIJI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA KATIKA ENEO LA MJIMWEMA YA MWAKA, 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Mipango Miji ya Kurasimisha Makazi yasiyopangwa Eneo la Mjimwema ya Mwaka, 2023.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililobainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango miji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina katika eneo la kwenye Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi wa Mji wa Makambako.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Unaanzia kwenye njiapanda ya barabara ya Njombe – Songea na bomba la Mafuta la Tanzania – Zambia - Mafuta (TAZAMA) kwenye majira – nukta 700553SM, 9021369KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kwa kufuata barabara ya Njombe – Songea hadi njiapanda ya Soko la Mbao kwa umbali wa kilomita 1.539 hadi majira – nukta 700415MS, 9019870KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki karibu na makaburi ya Magegere kwa umbali wa kilomita 0.993 hadi kwenye majira – nukta 701365MS, 9019584KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki kwa kufuata barabara ya Mpakani kwa umbali wa kilomita 0.669 hadi kwenye kalavati ambalo lipo kwenye majira - nukta 701624MS, 9020199KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Mashariki kwa kufuata eneo oevu kwa umbali wa kilomita 0.643 hadi bonde la Luligo kwenye majira - nukta 702065MS, 9020652KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi kwa umbali wa kilomita 1.097 hadi kwenye majira – nukta 701463MS, 9021506KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi kwa umbali wa kilomita 0.506 kuelekea bomba la mafuta la TAZAMA hadi kwenye majira – nukta 701071MS 9021787KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi kuelekea bomba la mafuta la TAZAMA kwa umbali wa kilomita 0.687 hadi ulipoanzia".

Dodoma,
……………, 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*